# Wadau wagawanyika mpango kufungwa Ziwa Tanganyika

Saada Amir, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Serikali imetangaza mpango wa kusitisha shughuli za uvuvi ndani ya Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu, huku wadau wakiibua maoni tofauti.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati wa mkutano wake na wadau wa uvuvi uliofanyika mkoani Kigoma na kwamba shughuli hizo zinatarajiwa kusitishwa kuanzia Mei 15 hadi Agosti 15, 2024.

Alisema hatua hiyo itasaidia samaki kuendelea kuzaliana na kuongeza tija kwa wavuvi, wanaofanya shughuli zao ndani ya ziwa hilo.

Waziri Ulega alisema hatua hiyo pia ni utekelezaji wa mkataba wa kikanda wa nchi wanachama wa mamlaka ya Ziwa Tanganyika, ambako nchi za Zambia, Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mwaka 2022 zilikubaliana kwa kanuni moja ya kuzitambua zana haramu za uvuvi.

"Pamoja na kufunga shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika, Serikali imeanza kutekeleza njia mbadala za kuwawezesha wananchi kujiendeleza kiuchumi, ikiwemo kukopesha vikundi maboti na vizimba kwa ajili ya miradi ya ufugaji wa samaki," alisema.

Katika hilo alisema tayari Serikali imetenga Sh200 milioni kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (Tafiri), kubainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki.

### Wadau watia neno

Mwenyekiti wa wavuvi mkoani Kigoma, Francis John alisema wamekubaliana na mpango huo unaokwenda kuokoa mazalia ya samaki na kupunguza vitendo vya uvuvi haramu.

Katibu wa Chama cha Wavuvi Tanzania (Tafu), Jephta Machandaro alisema anakubaliana na mpango huo kwa kuwa si tu utaendeleza rasilimali za uvuvi, lakini pia utalinda mazalia ya samaki.

Hata hivyo, katibu huyo alisema angepata nafasi ya kukutana na Ulega, angemshauri Serikali isitishe uvuvi wa dagaa ambao anaamini ndio unakomba hadi mazalia ya samaki na uvuvi wa samaki uendelee kwa kuwa unatumia nyavu rafiki.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Taasisi ya Muungano wa Wavuvi nchini (Fuo), Jevenary Mtagili alisema wavuvi wengi hawaukubali mpango huo na hata mwaka jana waliupinga

# Lake Tanganyika fishing to 'hibernate' for three months

By Guardian Reporter

THE government is preparing to suspend fishing activities in Lake Tanganyika for three months to enable fish to reproduce, thus raising fishing productivity subsequently.

Abdallah Ulega, the Fisheries and Livestock minister, told fishing stakeholders in Kigoma yesterday that the ban is slated for May 15 to August 15 as part of requirements set out in the Convention on the Sustainable Management of Lake Tanganyika.

The pact lays down measures and procedures for the sustainable management of fishing activities in the lake, he said, noting that a study conducted on the lake determined that there was vast shortage of fish and seafood in the lake.

The reason is largely an increase in unsustainable fishing causing the destruction of fish breeding grounds, he explained, adding that the government has started rolling out remedies, including alternative ways to enable people to to

TURN TO PAGE 2

CamScanner